Tomaso – Mtume

(Thomas – The Apostle)

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 15, 2011

Tomaso – Mtume

(Thomas – The Apostle)

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 15, 2011

Tomaso – Mtume

Yohana 20:19-20

Jina la Tomaso linatokea mara 12 katika Agano Jipya.

Mat. 10: 3; Marko 3:18; Luka 6:15; Yohana 11:16; Yohana 14:5; Yohana 20:24; Yohana 20:27; Yohana 20:28; Yohana 20:29; Yohana 21:2; Matendo 1:13.

"Tomaso" ni jina la Kiaramaic linalomanisha "pacha". Katika vifungu vitatu Yohana anamwonyesha kama "Pacha" ambalo ni neno ya Kiyunani likimanishaa "pacha". Wengi wanaamini kwamba hili lilikuwa jina lake la utani kwa sababu alikuwa pacha, wengine wanadhani kwamba linaweza kuwa jina lake la kweli. Aliitwa Pacha.

Katika Mat. 10:3, Tomaso analinganishwa na Mathayo. Katika Mdo. 1:13, analinganishwa na Filipo.

- Mat. 10:3, "*Filipo na Bartholomayo; Tomaso na Mathayo mtoza ushuru; Yakobo wa Alfayo, na Thadayo;*"
- Mdo. 1:13, "*Hata walipoingia wakapanda orofani, walipokuwa wakikaa Petro na Yohana, na Yakobo, na Andrea, Filipo na Tomaso, Bartholomayo na Mathayo, Yakobo wa Alfayo, na Simoni Zelote, na Yuda wa Yakobo.*

Katika Yohana 21:2-6, tunaona anaorodheshwa wa pili baada ya Petro.

Yohana 21:2-6, "*Simoni, na Tomaso aitwaye pacha, na Nathanaeli wa Kana ya Galilaya, na wana wa Zebedayo na wengine wawili wa wanafunzi wake, walikuwapo pamoja. Simoni Petro aliwaambia, naenda kuvua samaki. Nao wakamwambia sisi nasi tutakwenda nawe. Basi wakaondoka wakaapanda chomboni; ila usiku ule hawakupataa kitu. Hata asubuhi kulipokucha, Yesu alisimama ufuoni; walakini wanafunzi hawakujua ya kuwa ni Yesu. Basi Yesu akawaambia, wanangu mna kitoweo? Wakamjibu La. Akawaambia litupeni jarife upande wa kuume wwa chombo, nanyi mtapata. Basi wakatupa; wala sasa hawakuweza kulivuta tena kwa sababu ya wingi wa samaki.*"

Yawezekana Tomaso alikuwa mvuvi.

Labda mitume 7 kati ya 12 walikuwa wavuvi.

Tomaso hatajwi zidi ya wale 12 katika vitabu vingine vya injili, lakini Yohana anampa jukumu kubwa.

Yawezekana alikuwa mtume muhimu sana kuliko tunavyomchukulia mara nyingi.

Kimsingi anatuonyesha tabia ambazo tunatakiwa kuzingatia na zinatuonyesha kitu kuhusu tabia yake.

Tulipomtaja Ayubu, ghafla tunafikiri kuhusu "upole wa Ayubu"

Tunapomtaja Tomaso, ghafla tunafikiri kuhusu "Tomaso mwenye mashaka."

Lakini hili labda lisiwe sawa au njia sahihi tunayopaswa kumfikiria.

Tuangalie kidogo katika vifungu vya maandiko ambayo hutuambia vitu kuhusu Tomaso.

"Tomaso Shujaa"

Yohana 11:16, "*Basi Tomaso aitwaye Pacha, akawaambia wanafunzi wenziwe, twendeni na sisi ili tufe pamoja naye.*"

Yesu anataka kwenda Bethania, karibu na Yerusalemu. Yesu ameshatishiwa maisha na mitume wote wameshafahamu hatari ya Yesu kama akirudi katika eneo hilo.

- Yohana 10:22, "*Basi huko Yerusalemu ilikuwa Sikukuu ya Kutabaruku; ni wakati wa baridi.*"
- Yohana 10:31, "*Basi Wayahudi wakaokota mawe tena ili wampige.*"
- Yohana 10:39-40, "*Wakatafuta tena kumkamata; lakini akatoka mikononi mwao. Akaenda zake tena ng'ambo ya Yordani, mpaka mahali pale alipokuwapo Yohana akibatiza hapo kwanza, akakaa huko.*"

Wakati huo katika sura ya 9 ya kitabu cha Yohana baada ya Yesu kumponya kipofu hekaluni, Mafarisayo na Wazee wa baraza walipanga kumwua (sura za 9 & 10 ya Yohana).

Baada ya hili, Yesu anasikia habari kuhusu Lazaro.

Yohana 11:1-8, "*Basi mtu mmoja alikuwa hawezi, Lazaro wa Bethania, mwenyeji wa mji wa Mariamu na Martha, dada yake. Ndiye Mariamu yule aliyempaka Bwana marhamu, akamfuta miguu kwa nywele zake, ambaye Lazaro nduguye alikuwa hawezi. Basi wale maumbu wakatumaa ujumbe kwake wakisema, Bwana yeye umpendaye hawezi. Naye Yesu aliposikia,*

alisema ugonjwa huu si wa mauti, baali ni kwa ajili ya utukufu wa Mungu, ili Mwana wa Mungu atukuzwe kwa huo. Naye Yesu alimpenda Martha na umbu lake na Lazaro. Basi aliposikia ya kwamba hawezi, alikaa bado siku mbili pale pale alipokuwapo. Kisha baada ya hayo, akawaambia wanafunzi wake, Twendeni Uyahudi tena. Wale wanafunzi wakamwambia Rabi, juzi juzi tu Wayahudi walikuwa wakitafuta kukupiga kwa mawe, nawe unakwenda huko tena?"

Tomaso shujaa anatambua vitisho kwa Yesu kama akirudi katika eneo lile, lakini anakuwa MNARA WA NGUVU, na anaongoza njia, akisema, **"Sawa, kama wanaenda kumuua, twendeni tukafe pamoja naye!"**

Ujasiri kama huo na uongozi.

"Tomaso mtafutaji, na anayejifunza"

Yohana 14:5, "*Tomaso akamwambia Bwana, sisi hatujui uendako, nasi twaijuaje njia?*"

Angalia ya umaarufu, matendo yenye kufariji yanayofanywa na Yesu,

Yohana 14:1-4, "*Msifadhaike mioyoni mwenu; mnamwamini Mungu, niaminini na mimi. Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; kama sivyo ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi nanyi mwepo. Nami niendako mwaijua njia.*"

Lakini Tomaso anamwambia, "Bwana sisi hatujui uendako, [sasa] tutaijuaje njia?"

Tomaso sio mtu pekee anayekanganywa.

Hakunaa mtume yeyote aliyeelewa ambacho Yesu alikuwa akiliongelea.

Baadhi ya watu, wanaposhindwa kuielewa, wanabaki kimya na kuonekana kuwa wamekanganywa, lakini Tomaso tena anaongoza njia katika kutaka kujua hakika alichokiongelea , wanaposhindwa kuielewa, wanabaki kimya na kuonekana kuwa wamekanganywa, lakini Tomaso tena anaongoza njia katika kutaka kujua hakika alichokiongelea Yesu, na mahali alikokuwa akienda Yesu.

Hivyo tunamwona Tomaso kama mwanafunzi mwenye bidii, akihitaji na kutafuta ukweli, akitaka kuwa na hakika kwamba anamwelewa mwalimu wake.

Je hii siyo tabia ya kupongezwa na kusifiwa?

“Tomaso Mtaratibu Kuweza Kushawishika”

Yohana 20:19-24, “*Ikawa jioni siku ile ya kwanza ya juma, pale walipokuwapo wanafunzi, milango imefungwa kwa hofu ya Wayahudi; akaja Yesu akasimama katikati, akawaambia, amani iwe kwenu. Naye akiisha kuyasema hayo akawaonyesha mikono yake na ubavu wake. Basi wale wanafunzi wakafurahi walipomwona Bwana. basi Yesu akawaambia tenaa, amani iwe kwenu; kama Baba alivyonituma mimi, mimi nami nawapeleka ninyi. Naye akiisha kusema hayo akawavuvia, akawaambia, pokeeni Roho Mtakatifu. Wowote mtakaowaondolea dhambi, wameondolewa; na wowote mtakaowafungia dhambi, wamefungiwa. Walakini mmoja wa wale Thenashara, Tomaso aitwaye Pacha, hakuwako pamoja nao alipokuja Yesu.*”

Badala ya kumuita “Tomaso mwenye mashaka”, tunapaswa kumwona katika mtazamo mwingine.

Tomaso hakuwepo Yesu alipotokea mara ya kwanza – hatujui ni kwa nini!

Lakini badala ya kumuita “Tomaso mwenye mashaka,” hebu tumfikirie kama mtu ambaye asingedanganyika, au ambaye hakutaka kuongozwa vibaya; sio shakwe.

Hakuwa na “mashaka” kamwe kuliko mitume wengine waliokuwepo kabla ya Yesu kuwatokea.

Ni mtu anayetaaka uthibitisho!

Alitaka kuona ushahidi kwa macho yake mwenyewe!

Na tunapotamani nafasi yake ya kutaka uthibitisho, na kutaka ushahidi na siyo kudanganywa – **anafanya kosa katika njia moja muhimu!**

Kosa la Tomaso siyo kwamba alitaka uthibitisho, lakini kwamba alishindwa kukumbuka thamani ya shahidi wa macho.

Kama Tomaso hakutaka kuamini macho ya wengine, angewezaje kuwa na hakika kama angeweza kuyaamini macho yake mwenyewe?

Linakuja shauri la ni aina gani ya uthibitisho mtu ataukubali.

Hataivyo, Yesu, alitoa uthibitisho halisi ambao Tomaso alihitaji.

Yesu hakumdanganya, lakini alimkumbusha kwamba uthibitisho alioukataa ungetosha. Alipaswa kuwaamini wengine, ambao walikuwa mashahidi walioona.

Yesu alitoa baraka zake na sifa kwa wale waliopaswa kuamini kwa sababu ya ushahidi wa mitume hawa ambao walikuwa mashahidi walioona!

Yohana 20:29-31, "*Yesu akamwambia wewe kwa kuwa umeniona, umesadiki; wa heri wale wasioona, wakasadiki. Basi kuna ishara nyingine nyingi alizozifanya Yesu mbele ya wanafunzi wake, zisizoandikwa katika kitabu hiki. Lakini hizi zimeandikwa ili mpate kuamini ya kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu; na kwa kuamini mwe na uzima kwa jina lake.*"

Na Yesu alikuwa anaongea kuhusu sisi leo ni nani anayesoma ushahidi wao uliovuviwa!

Yohana anamfanya Tomaso kuwa binadamu halisi; na kifungu katika Yohana 20:25 inafunua tabia nyingine kuu.

"Tomaso anayependa na Muwajibikaji"

Yohana 20:25, "*Basi wanafunzi wengine wakamwambia, tumemwona Bwana. akawaambia, mimi nissipoziona mikononi mwake kovu za misumari, na kutia kidole change kaatika mahali pa misumari, na kutia mkono wangu katika ubavu wake, mimi sisadiki haataa kidogo.*"

Tunafahamu kwamba Tomaso aliongelea kuhusu kutia vidole vyake kwenye vidonda vya Yesu, na Yesu akamwonyesha vidonda, lakini hatuambiwi kama Tomaso alinyoosha mikono yake na kumgusa.

Hataivyo, niwazi kwamba mitume wote walimgusa Yesu – alikuwa halisi.

1 Yohana 1:1-3, "*Lile lililokuwako tangu mwanzo, tulilolisikia, tuliloliona kwa macho yetu, tulilolitazama, na mikono yetu ikalipapasa, kwa habari ya neno la uzima; (na uzima huo ulidhihirika, nasi tumeona, tena twashuhudia, na kuwahubiri ninyi ule uzima wa milele, uliokuwa kwa Baba, ukadhihirika kwetu); hilo tuliloliona na kulisikia, twawahubiri na ninyi; ili nanyi mpate kushirikiana nasi: na ushirika wetu ni pamoja na Baba, naa pamoja na Mwana wake Yesu Kristo.*"

Yohana alifahamu umuhimu wa toba hii ya imani – na wa wajibu huu wa Yesu.

Yawezekana hii ndiyo sababu ya Yohana amekuwa akimpa Tomaso utambuzi mbele ya hili wa sehemu muhimu alioucheza katika umitume wa Yesu.

Pale anapotufunulia ujasiri wa Tomaso huyu.

Yohana 11:16, "*…Twendeni na sisi, ili tufe pamoja naye.*"

Na Tomaso mwaminifu, mtafutaji.

Yohana 14:5, "*…Bwana sisi hatujui uendako, nasi twaijuaje njia?*"

Hataivyo kifungu kikuu hapa ni Yesu, akimjibu Tomaso katika vs. 29.

Yohana 20:29, "*Yesu akamwambia wewe kwa kuwa umeniona, umesadiki; waheri wale wasioona, wakasadiki.*'

Yesu anasema ushahidi wa kuamini ushahidi wa macho unatosha kufanya waumini, na watu kama hao watabarikiwa.

Kama hatuwezi kuamini huyu shahidi wa macho anayepatikana, siyo tu kwamba tunapaswa kuyaamini macho yetu wenyewe.

Hii inafanana sana na kauli ya Yesu katika Luka 16:31.

Luka 16:31, "*Akawaambia wasipowasikia Musa na manabii, hawatashawishwa haata mtu akifufuka katika wafu.*"

Yohana anatuambia kusudi lake binafsi la kuandika waraka huu katika mistari inayofuata:

Kufanya waumini, Yohana 20:31, "*Lakini hizi zimeandikwa ili mpate kuamini ya kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu; na kwa kuamini mwe na uzima kwa jina lake.*"

Na kutoka katika kauli ya Bwana mwenyewe, wale wanaoamini ushahidi ulioandikwa wenye sifa, ushahidi unaoaminiwa wa hawa mitume wa mashahidi wa macho anaweza kuwa na uzima wa milele.

Yohana 20:30-31, "*Basi kuna ishara nyingine nyingi alizozifanya Yesu mbele ya wanafunzi wake, zisizoandikwa katika kitabu hiki. Lakini hizi zimeandikwa ili mpate kuamini ya kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu; na kwa kuamini mwe na uzima kwa jina lake.*"